cha chini cha samaki wazazi katika Bwawa la Mtera

# Wabunge wafichua siri kupungua samaki katika mabwawa, maziwa

**Na MUSSA YUSUPH,** *Dodoma*

UTAFITI umebaini kupungua kwa kiwango kikubwa cha samaki katika maziwa, mabwawa na mito nchini hali iliyosababishwa na usimamizi hafifu wa rasilimali hizo.

Imebainika kuwa katika Ziwa Victoria samaki wazazi wapo chini ya asilimia 0.4, huku katika Bwawa la Mtera samaki wakipungua na waliopo wamekumbwa na udumavu.

Akizungumza bungeni jijini hapa juzi, taarifa ya shughuli zilizotekelezwa na Kamati ya Kudumu ya Bunge, Kilimo, Mifugo na Maji, kuanzia Februari 2022 hadi Januari 2023, mwenyekiti wa kamati hiyo, Christine Ishengoma, alisema hali hiyo imesababishwa pia na uwekezaji mdogo wa utafiti na teknolojia ya kisasa.

"Upungufu huo umeathiri upatikanaji wa malighafi za viwanda vya kusindika minofu ya samaki, watu kupoteza ajira, kukosekana kwa lishe na kuvuruga uchumi wa wavuvi," alisisitiza.

**UTAFITI UNAVYOELEZA**

Mwenyekiti huyo wa kamati alisema kwa mara ya kwanza katika kipindi cha miaka 30, Taasisi ya Utafiti wa Uvuvi nchini (TAFIRI), ilifanya utafiti kuhusu wingi na mtawanyiko wa samaki katika Ziwa Tanganyika kwa fedha za maendeleo za ndani.

Alisema utafiti huo ulibaini Ziwa Tanganyika, upande wa Tanzania kuna kiasi cha tani 138,500 za samaki wanaojumuisha dagaa, migebuka na aina zingine ambapo utafiti huo ulifanyika kipindi cha masika Februari na Machi mwaka jana.

Pia, kupitia Jumuiya ya Afrika Mashariki (EAC), alisema TAFIRI imeshirikiana na Shirika la Uvuvi la Ziwa Victoria (LVFO), kufanya utafiti wa wingi, bioanuwai na mtawanyo wa samaki katika Ziwa Victoria.

Alieleza kuwa, utafiti huo ulibaini wingi wa sangara umepungua kwa takribani asilimia 50, kutoka tani 1,024,623 mwaka 2020 mpaka tani 502,919 mwaka 2021.

**BUNGE LASHAURI**

Kwa sababu hiyo, alisema Bunge linashauri serikali kuwekeza katika utafiti na teknolojia ya uzalishaji wa samaki na viumbe maji wengine.

Pia, Bunge liliitaka serikali iiwezeshe TAFIRI kupata meli ya uvuvi itekeleza majukumu ya kiutafiti katika ukanda wa maji ya bahari, kutenga fedha na kuwawezesha wafugaji wa samaki kwa njia ya vizimba katika mabwawa na maziwa, kwa lengo la kuongeza uzalishaji.

"Serikali idhibiti uvuvi haramu kwa kutumia njia sahihi ambazo hazitwezi utu wa wananchi lakini zinaleta matokeo chanya, ihamasishe sekta binafsi kuwekeza katika uzalishaji wa samaki na vyakula vya samaki," ilifafanua taarifa ya kamati.

Taarifa iliongeza kuwa: "Serikali iimarishe huduma za ugani kwa kuwapatia maofisa ugani utaalamu na vifaa vya ukuzaji wa viumbe maji, kwani wananchi wamehamasika kufuga samaki katika vizimba lakini hakuna wataalamu wa kutosha kuwasaidia mbinu bora za ufugaji."

Mwenyekiti wa kamati alishauri serikali ifanye marekebisho ya Sheria ya Kitengo cha Kulinda Uhifadhi wa Rasilimali za Uvuvi Baharini, kwa kukiwezesha kusimamia uhifadhi wa rasilimali za uvuvi katika maji baridi kwa lengo la kulinda sehemu za mazalia ya samaki.

Alisema mapendekezo hayo yanatokana na ukweli kwamba, kitengo hicho kilifanikiwa kwa sehemu kubwa kudhibiti uvuvi wa kutumia mabomu katika Bahari ya Hindi.

Ishengoma ambaye pia ni Mbunge huyo wa Viti Maalumu (CCM), alisema kamati inatambua kwamba serikali imejielekeza kuongeza uwekezaji na uzalishaji mkubwa wa viumbe maji kwa kutumia fursa ya uwepo wa rasilimali za maji zilizopo katika bahari, maziwa, mabwawa, mito na mabonde oevu.

Aliongeza, kamati pia imebaini uzalishaji wa vifaranga bora vya samaki bado upo chini kwa sababu ya changamoto mbalimbali kama uhaba wa zana, teknolojia za kisasa, huduma duni za ugani na uwekezaji mdogo.

ZIMAMOTO